

Unukuzi wa Utafiti wa Uchunguzi wa Visa vya COVID-19 Mtandaoni

[muziki wa kuchangamsha]

[Masimulizi] Uchunguzi wa visa ni njia ya kupunguza kuenea kwa COVID-19

Wafanyakazi wa afya waliofundishwa huwasiliana na watu ambao wamepimwa na kupatikana na virusi vya COVID-19 na kuwauliza maswali ili kujua watu wengine ambao walikaa karibu nao. Watu hawa waliokaribiana sasa wanaweza kuwa na COVID-19 na wanapaswa kukaa nyumbani.

Kawaida, mahojiano ya uchunguzi kuhusu visa hufanywa kwa njia ya simu. Sasa, una fursa ya kujibu maswali hayohayo katika utafiti wa kibinafsi, mtandaoni.

Kilicho bora zaidi? Ikiwa ulishiriki nambari yako ya simu wakati ulikuwa unapimwa, tutakutumia ujumbe mfupi kukujulisha unaweza kushiriki kwenye utafiti!

Kwanza, tutawasiliana nawe. Unaweza kujibu kwa kuchagua 1, 2, 3, au 4 kulingana na lugha unayofahamu vizuri zaidi. Tutakuuliza anwani ya barua pepe na tutume kiungo cha utafiti moja kwa moja kwenye kikasha chako. Usipojibu ujumbe huo, utapigiwa simu na mfanyakazi wa afya.

Unaweza kuchukua muda wako kujaza utafiti. Mwishowe, utapokea maelezo muhimu kuhusu jinsi ya kupunguza hatari ya kupitisha COVID-19 kwa wengine, na maelezo kuhusu rasilimali za mitaa ambazo zinaweza kupatikana kwako kwa vitu kama mboga na dawa.

Idara ya afya inachukulia faragha yako kwa uzito sana. Hatutawahi kukuuliza utupe pesa, maelezo ya benki, au Nambari yako ya Bima ya Jamii.

Ikiwa ulipatikana na virusi na una maswali, unaweza kupigia simu 651-201-5689 ili uzungumze na mfanyakazi wa afya.

[muziki wa kuchangamsha]

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

1/28/21 (Swahili)

Ili kupata maelezo haya kwa muundo tofauti, pigia simu: 651-201-4989